Miaka 4 ya Dk. Shein

TUNAJIVUNIA AMANI, UTULIVU NA MAENDELEO

Maoni yetu

Tunajivunia amani, utulivu na maendeleo

Wananchi wa Zanzibar wanayo kila sababu ya kusherehekea mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne (4) tokea kuundwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa, licha ya baadhi ya changamoto zilizojitokeza ndani ya kipindi hicho. Ni dhahiri mafanikio hayo yanatokana na uongozi wa busara, amani, utulivu na uvumilivu wa kisiasa.

Chini ya muundo huo wa Serikali, wananchi wameshuhudia mambo mengi ambayo yataendelea kugusa maisha yao ya kila siku na kubaki kuwa historia ndani ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Ni dhahiri wapo baadhi ya wanaharakati na wafuatiliaji wa masuala ya kisiasa na maendeleo ya Zanzibar, ambao hawakuwa na matumaini makubwa na mfumo huo, wakiamini kwamba matatizo ya kisiasa ya Zanzibar ni donda ndugu ambalo haliwezi kutibika.

Aidha, wapo baadhi ya wananchi walioelezea wasiwasi wao juu ya uwezekano wa kuiendesha Serikali ya awamu ya saba ambayo kwa maoni yao ni kubwa kuliko uwezo wa Serikali yenyewe.

Lakini busara, hekima na uvumilivu wa kisiasa wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein vimeithibitishia Zanzibar na dunia nzima kwamba, kila kitu kinawezekana iwapo kiongozi atakuwa na dhamira ya kweli ya kutekeleza aliyojipangia na hatimaye kufikia malengo aliyojiwekea.

Mafanikio ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa yanaweza kupimwa kutokana na utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2010 - 2015 ambayo inakwenda sambamba na Mpango Mkuu wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA II), Dira 2020 na Malengo ya Milenia, ambayo kwa mujibu wa taarifa za Tume ya Mipango kuna mafanikio makubwa yamepatikana kwenye maeneo hayo kwa upande wa Zanzibar.

Utulivu wa kisiasa amani na hatua kubwa ya maendeleo katika sekta mbali mbali yaliyopatika katika kipindi cha miaka minne tu baada ya miaka 15 ya mfarakano na uhasama wa kisiasa miongoni mwa wananchi wa Zanzibar yataendelea kukumbukwa milele.

UKUAJI WA UCHUMI

Miaka 4 ya Dk. Shein madarakani

- Uchumi wa Zanzibar Umekua kutoka 6.4 hadi 7.4
- Pato la Mtu binafsi limevuka lengo lililowekwa
- Idadi ya Watalii imeongezeka
- Makusanyo ya Kodi yameongezeka zaidi ya maradufu

Dk. Ali Mohamed Shein
Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti
wa Baraza la Mapinduzi

Mafanikio ya Serikali katika utekelezaji wa mipango na sera za nchi yanapimwa kutokana na vigezo mbali mbali ikiwemo ukuaji wa pato la taifa. Rasilimali fedha ni moja kati ya mambo yanayopewa uzito mkubwa katika kupima uimara wa Serikali siyo tu katika ukusanyaji, lakini pia namna ya fedha hizo zinavyotumiwa. Hii inatokana na ukweli kwamba, Serikali yoyote duniani haiwezi kuendeshwa kwa ufanisi bila ya kuwa na rasilimali fedha.

Uchumi wa Zanzibar umekuwa ukikua kila mwaka ambapo ulikuwa kwa asilimia 6.4 mwaka 2010 kufikia 7.4 mwaka 2014.

Kadhalika, Pato la Mtu Binafsi lilikuwa Tsh. 726,000 mwaka 2010. Maelezo ya Ilani ya CCM 2010 yalilenga alau lifikie Tsh 884,000/- ifikapo mwaka 2015. Katika mwaka 2013, Pato la Mtu Binafsi limefikia Tsh. 1.077 milioni.

Biashara ya usafirishaji na uingizaji wa bidhaa umezidi kuimarika na hasa usafirishaji wa karafuu na mwani kutoka Tsh. Milioni 17,907 mwaka 2010 hadi kufikia Tsh. Milioni 82.917 mwaka 2013.

Ndani ya kipindi cha miaka minne mafanikio makubwa yamepatikana katika sekta hii ya kiuchumi. Idadi ya watalii waliofika nchini kutoka 119,365 mwaka 2010 hadi kufikia watalii 181,242 mwaka 2013.

Mwaka 2010 wakati Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipokuwa inaingia madarakani, taasisi zinazoshughulikia makusanyo ya fedha nchini Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA) zilikuwa zikikusanya wastani wa Tsh. Bilioni 13 na 14 kwa mwezi. Kiasi hicho cha fedha kimekuwa kikiongezeka siku hadi siku na kufikia wastani wa Tsh. Bilioni 30 kwa mwezi mwaka 2014. Hatua hii ni kubwa na zinastahiki kupongezwa.

Ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na matumizi mazuri ya fedha hizo, Kamati ya ukomo ya Wizara ya Fedha imekuwa ikichukua uangalifu mkubwa katika kugawa rasilimali hiyo, ikizingatia maeneo maalum kwa mujibu wa vipaumbele vya Serikali.

Hatua hiyo imeleta mafanikio makubwa katika kuimarisha uchumi wa nchi kwa kujenga miundombinu imara ya barabara, uwanja wa ndege, umeme, maji safi na salama na vile vile kuimarisha ustawi wa jamii ya Wazanzibari.

Sekta ya Elimu

Uzinduzi wa Mradi wa Elimu wa Karne ya 21 tarehe 28 Februari, 2012

Imekuwa jambo la kawaida katika miaka ya karibuni kuwaona wanafunzi wa elimu ya msingi, sekondari na elimu ya juu Zanzibar, mjini na vijijini kusoma kwa kutumia kompyuta, hali inayoashiria kufanikiwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutekeleza dhamira yake ya kusisitiza matumizi ya Sayansi na Teknolojia ili kuongeza ufanisi katika kazi. Hatua hiyo inakwenda sambamba na kukamilika ujenzi wa Skuli kadhaa za kisasa, maabara na maktaba za kisasa mjini na vijijini.

Umuhimu wa Elimu ni miongoni mwa masuala ambayo yalitambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kabla na baada ya Mapinduzi matukufu ya tarehe 12 Januari i964. Inaaminika kwamba suala hilo ni miongoni mwa sababu zilizopelekea kufanyika kwa Mapinduzi na ndio maana mara tu baada ya Mapinduzi Serikali ilitangaza elimu bure miongoni mwa wananchi wote wa Zanzibar bila ya kujali aina yoyote ya ubaguzi.

Kwa kutambua ukweli huo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kipindi cha miaka mitano 2010 - 2015 chini ya uongozi wa Chama Cha Mapinduzi CCM imeendelea kutoa kipaumbele cha kwanza

Darasa maalum la Kompyuta liliopo katika skuli mpya ya Sekondari ya Kiembe Samaki

kwa sekta ya elimu ikizingatia zaidi suala la elimu ya Sayansi na teknolojia.

Taarifa za Wizara hiyo zimeeleza kuwa, hali halisi ya utendaji katika kipindi cha miaka minne ya awamu ya saba inaridhisha sana na kuna maendeleo mengi yaliyopatikana.

Miongoni mwa mafanikio makubwa yanayohesabiwa ndani ya Wizara hiyo ni ujenzi wa Madarasa mapya 582 , maktaba, vyumba vya mitihani, vyumba vya kompyuta, madawati 8,370, seti ya viti na meza 2,237 na matengenezo skuli zaidi ya 30.

Hatua hiyo imefikiwa kutokana na dhamira iliyowekwa ndani ya Ilani ya CCM 2010 - 2015 ya kuhamasisha wananchi kushiriki katika ujenzi wa skuli mpya na kuongeza idadi ya madarasa katika skuli zilizopo kwenye maeneo yao. Lengo ni kwenda sambamba na ongezeko la watoto wanaohitaji kuandikishwa katika elimu ya msingi.

Maktaba ya Skuli mpya ya Sekondari ya Chasasa Pemba tarehe 23 Disemba, 2013

Elimu ya Amali

Sekta ya Kilimo na Maliasili

Ziara za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwenye mabonde ya mpunga kujionea mwenyewe shughuli zinavyoendelea, zimekuwa zikiwashajiisha wananchi na kuwatia ari ya kukamilisha malengo yao na malengo ya taifa. Aidha, ziara hizo zimekuwa zikiwafanya watendaji kuwa makini zaidi katika utekelezaji wa majukumu yao, wakijua kuwa katika ulimwengu huu wa ukweli na uwazi, chochote kinaweza kuzungumzwa mbele ya Rais wakati anapokuwa kwenye ziara zake hizo.

"MAPINDUZI ya Kilimo" ndio mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya saba wenye nia na shabaha ya kutekeleza kwa vitendo dhamira ya kuwakomboa wakulima wa Zanzibar kutoka katika kilimo duni kisichokuwa na tija na kuweka mazingira bora ya uzalishaji kwa kutumia utaalamu na vifaa vya kisasa.

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili katika kipindi cha mwaka 2010/2014 imetekeleza dhamira ya Mapinduzi ya kilimo kwa kutekeleza mikakati mbali mbali ikiwa ni pamoja na kutekeleza mkakati wa uimarishaji wa zao la karafuu ikiwemo utafiti, uzalishaji, usarifu na "branding" kwa kushirikiana na Wizara inayosimamia Biashara.

Katika jitihada za kuliendeleza zao la karafuu, jumla ya miche 1,694,328 Unguja na Pemba. Miche 921,647 imetolewa na kusambazwa kwa wakulima kwa ajili ya kupandwa mashambani bila ya malipo.

Aidha, tathmini imefanyika na matokeo yanaonesha mikarafuu iliyoota kwa Unguja ni asilimia 37 na Pemba ni asilimia 51.

Mavuno ya zao la Karafuu nchini yameongezeka kutoka tani 4,853 mwaka 2011/2012, tani 1,503 mwaka 2012/2013 na tani 5,374 mwaka 2013/2014. Kiasi hicho ni sawa na ongezeko la wastani wa tani 3,910 kwa mwaka, ambapo wastani wa tani 2,900 tu ndizo zilizokuwa zikivunwa katika miaka ya 2000.

Huduma za kilimo cha matrekta ilitekelezwa kwa mafanikio makubwa baada ya kufanikisha ununuzi wa Matrekta mapya 23 kutoka SUMA JKT - Tanzania Bara na kugaiwa kwa wakulima Unguja na Pemba. "Combine harvesters" 14 zimenunuliwa pamoja na kuyafanyia matengenezo matrekta 37 kwa ajili ya ukulima wa 2012/2013 na 2013/2014.

Jumla ya mitego 12,644 ya kunasia nzi waharibifu wa matunda imesambazwa kwa wakulima, Unguja na Pemba (mitego 5,730 Unguja na 6,914 Pemba). Pia mitego 9,320 ya nzi waharibifu wa matunda imebadilishwa dawa. Wizara inaendelea kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji maji kwa kipindi chote kuanzia mwaka 2010 hadi 2014 ambapo jumla ya mita 1,200 za misingi mikuu ya umwagiliaji maji imejengwa kwa saruji, mita 2,000 za udongo.

Mita 500 za miundombinu ya umwagiliaji maji

imejengwa kwa kiwango cha saruji katika bonde la Bumbwisudi. Hatua hii imewezesha kufikia eneo la hekta 800 lililoimarishwa miundombinu ya umwagiliaji maji.

Majaribio matatu ya kuzalisha mbegu aina ya SUPA BC yameanzishwa Kizimbani, Ole na Bumbwisudi na yamefikia hatua ya kuchanua. Mafunzo ya wakulima 400 kwa jaribio la aina mpya za mbolea (UDP na Yaramila) kwa zao la mpunga yamekamilika. Mafunzo mengine kwa wakulima 2,000 yameanza msimu wa Masika 2014.

Majaribio 6 ya viazi vitamu yameanzishwa katika maeneo ya Bambi, Kizimbani na Kilombero kwa Unguja na Makangale, Mjimbini na Matangatuani kwa Pemba. Tafiti 2 zimefanyika zikihusisha aina saba na aina sita za mbegu za mihogo ambazo zinaendelea shambani. Aidha, tafiti zimefanyika na aina 15 ya mbegu za viazi vitamu zimechaguliwa na wakulima kwa uchunguzi.

Uhifadhi wa mbegu 36 za kienyeji na za kigeni pamoja na jaribio la mbegu mbali mbali za tungule unaendelea, pamoja na Kazi za ujenzi na ukarabati wa maabara za (usarifu wa mazao, tissue culture na

udongo) zimekamilika.

Chuo cha Kilimo Kizimbani kimeimarishwa zaidi kwa lengo la kutoa huduma bora zaidi za elimu kwa wakulima kupitia mabwana shamba, Skuli za wakulima na maafisa wilaya. Chuo kimesajili wanafunzi 140 kwa mafunzo ya Kilimo ngazi ya cheti na wanafunzi 50 ngazi ya Diploma. Aidha, Chuo kiliendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 25 wa Diploma na 145 wa ngazi ya Cheti wanaendelea.

Katika kuimarisha mashirikiano na vyuo vya nje ya nchi, ziara kati ya chuo cha Kilimo Kizimbani na University of Life Science - Norway zimefanyika na makubaliano ya mashirikiano yameanza kutekelezwa.

Kwa kupitia Programu ya ASSP/ASDP-L jumla ya skuli 1,200 za wakulima zimeanzishwa (133 kila wilaya) ambazo zinajumuisha kaya za wakulima 35,000 nchini. Skuli hizo zimeanzishwa kwa lengo la kuimarishwa mafunzo ya aina mbali mbali na kupatiwa misaada ya kujiongezea kipato vikiwemo baskeli, mashine za kusagia muhogo, kuchujia asali, mashine za kutotolea vifaranga, kusafishia maziwa, ng'ombe na mbuzi wa maziwa, madume, Majogoo,

chanjo za mifugo na mbegu za majimaji kwa ajili ya kuzalisha ng'ombe chotara.

Kwa kipindi cha miaka minne Wizara kupitia Idara ya Chakula na Lishe pia imeweza kutekeleza kazi ya kukamilisha Miongozo ya uendeshaji wa Hifadhi ya Chakula (Operational Procedure Manual), kukamilisha taratibu za ukusanyaji wa taarifa za takwimu sambamba na 'database' ya uhakika wa chakula na lishe na taarifa husika zimeanza kuingizwa.

Jumla ya miche 3,556,869 ya misitu pamoja na miche 365,920 ya aina za viungo katika vitalu vya serikali imeoteshwa.

Jumla ya miche 2,098,072 inayojumuisha miche ya misitu 1,778,810 na matunda 319,262 imesambazwa kwa ajili ya upandaji katika mashamba ya serikali, barabarani, maeneo yaliyoathirika kwa uchimbaji wa mchanga na wanajamii kwa ujumlakwa mwaka 20013/2014.

Hekta 208 zimepandwa miti ya misitu katika mashamba ya Serikali (Unguja hekta 152.2 na Pemba hekta 10). Elimu ya uhifadhi wa misitu na uzinduzi wa kikundi cha uhifadhi wa Mikoko cha Fuoni Kibondeni pamoja na tathmini za athari zinazoweza kutokea kwenye mikoko baada ya kuazishwa kiwanja cha Gofu huko Mangapwani imefanyika.

Haya ni miongoni mwa juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Wizara yake ya Kilimo na Maliasili chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein.

Kauli za Mabalozi na Washirika wa maendeleo

Mabalozi wa nchi za Ulaya walioko Tanzania

Mabalozi na washirika wa maendeleo kutoka mataifa na mashirika mbali mbali ya kimataifa katika nyakati tofauti wamekuwa wakimtembela Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kubadilishana naye mawazo kuhusiana na mafanikio na changamoto za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa ambapo wengi wao wamesifu hatua iliyofikiwa.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa chini ya Rais wake Dk. Ali Mohamed Shein imetimiza miaka minne sasa tangu ilipoingia madarakani tarehe 3 Novemba 2010. Serikali hii ilivuta hisia za aina yake miongoni mwa wafuatiliaji wa masuala ya siasa Barani Afrika na duniani kote. Kutokana na historia ya kisiasa Zanzibar, waliowengi wakiwemo mabalozi na washirika wa maendeleo hawakuwa na matarajio makubwa ya mafanikio ya mfumo huo wa kisiasa. Miaka minne sasa imepita tokea wakati huo; nini maoni ya mabalozi na washirika wa maendeleo?

Malengo ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa kiasi kikubwa yametimizwa hatua ambayo imewaridhisha washirika wa maendeleo na kuahidi kusaidia katika nyanja mbali mbali ikiwemo miradi ya maendeleo na uchumi pamoja na ustawi wa jamii.

Balozi wa Marekani Mark Childress akizungumza

na Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein Ikulu alisema Marekani imefurahishwa na kuwepo kwa mazingira ya amani na utulivu tangu ilipoundwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

"Serikali ya Marekani imefurahishwa na mazingira yaliopo visiwani ya amani na utulivu kufuatia kuwepo kwa Serikali ya umoja wa kitaifa……matumaini yetu makubwa viongozi waliopo madarakani watafanya kazi kwa mashirikiano"alisema.

Aliyekuwa Mwakilishi wa Jumuiya ya Ulaya (EU) nchini Balozi Filibe Sebriga alisema amefurahishwa na amani iliyopo Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo imewaunganisha wananchi wote.

"Jumuiya ya Ulaya kama wadau wakubwa wa maendeleo ya Zanzibar tumefurahishwa na muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa iliopo ambapo sisi tunaamini kwamba ndiyo ufumbuzi na suluhu ya matatizo ya kisiasa Zanzibar" alisema.

Balozi wa Ujarumani nchini Tanzania Egon Kochanke ambaye alifika Ikulu ya Zanzibar kufanya mazungumzo na Rais wa Dk. Ali Mohamed Shein alisema amefurahishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa inayoundwa na vyama viwili vya siasa CCM na CUF ambayo imemaliza siasa za chuki na uhasama uliodumu kwa muda mrefu.

"Ujarumani imeridhishwa na mazingira yaliopo nchini ya utulivu wa kisiasa ambayo yanatoa nafasi ya kupiga hatua kubwa ya maendeleo na kupunguza umasikini ambapo sisi tupo tayari kufunguwa milango ya ushirikiano katika sekta mbali mbali ikiwemo utalii". alisema.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kusaidia maendeleo ya wakulima na wafugaji (IFAD) Perin Saint Ange alisema Shirika lake litaendelea kusaidia miradi miwili ule wa ASSP wa kuendeleza wakulima pamoja na ASP kwa upande wa wafugaji kuona kwamba wanaondokana na mbinu za kizamani za ufugaji na ukulima.

Norway ambayo ni mdau mkubwa wa maendeleo ya

Balozi wa Marekani nchini Tanzania akiwa na Rais - Ikulu

Mratibu Mkaazi wa UN Alberic Kacou akiwa na Rais - Ikulu

Ujumbe wa Wawekezaji kutoka nchini Uholanzi

Zanzibar katika nishati ya umeme imesema Serikali ya umoja wa kitaifa imekuja kuleta maendeleo na kuondosha migogoro na malumbano ya kisiasa.

"Norway imeamua kurudisha misaada yake kwa Zanzibar baada ya kufikiwa kwa makubaliano ya kisiasa yenye lengo la kuondosha siasa za malumbano na mivutano.....sasa huu ni wakati muafaka wa kufikiwa kwa maendeleo" alisema wakati alipokuwa akikagua barabara za Pemba.

Waziri mkuu wa Finland Jyrki Katainen alisema nchi yake ambayo inagharamia mradi wa SMOLE ambao unajishughulisha na uhifadhi wa ardhi na mazingira pamoja na kulinda misitu ya asili imeridhishwa na matumizi ya misaada yake.

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kutunza watoto UNICEF Dorothy Rozga amesema amefurahishwa jinsi Zanzibar inavyozingatia haki za watoto kwa mujibu wa mikataba ya Kimataifa.

"Nimefurahishwa na mikakati ya kutunza watoto kwa kuwapatia maeneo maalumu huku vifo vya akinamama vinavyotokana na uzazi vikipunguwa" alisema.

Waziri wa Biashara wa nje kutoka Uholanzi Bibi Liliane Ploume ambaye alifika Zanzibar akiwa na ujumbe wa wawekezaji wapatao 50 kutoka nchini kwake alisema wamefurahishwa na mazingira ya uwekezaji yaliopo Zanzibar na zaidi ni kuwepo kwa amani na utulivu.

Nae muakilishi wa Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) Bw. Alberic Kacou amesema shirika lake litaendelea kufanyakazi kwa pamoja na SMZ ili kufanikisha jitihada zake za kupambana na umasikini na kufikia malengo ya milenia.

Sekta ya Afya

Kukamilika kwa ujenzi wa bohari kuu ya dawa Maruhubi, ujenzi wa vituo vipya vya afya katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba, uwekaji wa vifaa vya kisasa kwenye hospitali kadhaa ikiwemo hospitali kuu ya Mnazi Mmoja, kuhitimu kwa wanafunzi wa Chuo cha kwanza cha tiba ya Afya, uamuzi wa kukipeleka Chuo cha Afya chini ya utawala wa SUZA pamoja na jitihada za Serikali za kutafuta wawekezaji, ni miongoni mwa mambo ambayo hatimaye yataifanya Zanzibar kupiga hatua kubwa katika sekta ya afya ikilinganishwa na nchi nyingi za Bara la Afrika.

Imebainika wazi kwamba tokea Mapinduzi ya Januari 1964, juhudi maalum zimekuwa zikichukuliwa na Serikali za kupatikana madaktari wa kutosha, kuongeza wafanyakazi wapya wa afya, kuwapa dhamana za kazi muhimu na kuwaandalia mafunzo kwa ajili ya kuendeleza kazi zao.

Katika matukio na nyakati tofauti, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amekuwa akisema kuwa wananchi wa Zanzibar wanayo kila sababu ya kufurahia mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta ya afya. Ukiacha mambo ya jumla ambayo yameendelea kutekelezwa tokea awamu zilizopita, kama vile ujenzi wa vituo 134 vya afya ambavyo vimepelekea kupunguza masafa ya kutembea kupata huduma hadi kufikia chini ya wastani wa kilomita tano, huduma za afya zimeimarishwa pia kwenye maeneo na viwango tofauti;

Hospitali nne za koteji ambazo kila hospitali ina vitanda 40 na huduma muhimu zikiwemo huduma za uchunguzi wa maabara, huduma za meno, upasuaji mdodo na kadhalika zimeimarishwa zaidi .

Kuanzishwa kwa “Zanzibar Medical School” kwa utaratibu maalum mnamo mwaka 2007 ikiwa na wanafunzi 40, kwa mashirikiano na Chuo Kikuu cha

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akishuhudia ubadilishanaji hati baada ya kutiwa saini makubaliano baina ya Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dk. Saleh Mohamed Jidawi na Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Manipal Bw. Rajen Padukone katika shughuli iliyofanyika tarehe 06 Februari, 2014 mjini Bungalore nchini India. Makubaliano hayo yatawanufaisha Madaktari wa Zanzibar kwenda kujifunza kazi katika Chuo cha Hospitali hiyo

Matanzas cha Cuba, ni miongoni mwa jitihada za Serikali kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo sugu la madaktari hapa Zanzibar. Wanafunzi wengine 12 ambao wanakaribia kumaliza mafunzo yao walijiunga na Chuo hicho baadae.

Tukio la kuhitimu madaktari 38 kwa wakati mmoja linaonekana kuwa ni tukio kubwa la aina yake. Hayo ni mafanikio makubwa siyo tu kwa kuwa Serikali imeweza kutoa idadi kubwa ya madaktari kwa wakati mmoja lakini kubwa zaidi ni kwa madaktari ha kupata mafunzo yao katika Chuo cha Madaktari cha Zanzibar kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Matanzas cha nchini Cuba.

Takwimu zinaonesha kuwa uwiano wa daktari kwa idadi ya watu umekuwa ukiimarika kwa kadri nchi inavyoendelea. Katika mwaka 1992 uwiano ulikuwa daktari mmoja kwa wananchi 58,000. Hadi mwezi Januari mwaka 2014, wakati Zanzibar inaadhimisha Miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya 1964, uwiano wa daktari kwa idadi ya watu ulikuwa ni daktari mmoja kwa wananchi 18,982.

Uwiano huo utakuwa bora zaidi katika kipindi kifupi kijacho, hasa baada ya Serikali kuwaajiri madaktari wapya 38 na watakaporejea masomoni vijana wengine wengi waliopo Tanzania Bara, China, Urusi, Ukraine na kadhalika.

Vile vile Serikali ina matarajio makubwa ya kupunguza idadi ya watu wanaohudumiwa na daktari watakapomaliza mafunzo yao wanafunzi waliojiunga mwaka jana katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Iko kila ishara kuwa katika miaka michache ijayo Serikali itaweza kufikia uwiano unaopendekezwa na Shirika la Afya Duniani wa angalau watu elfu kumi (10,000) kwa daktari mmoja kwa nchi zinazoendelea.

Katika kulishughulikia tatizo la kutokuwa na kitivo cha utibabu (Faculty of Medicine/School of Medicine), mwezi wa Mei, mwaka 2012 Serikali

ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kuanzisha Skuli ya Sayansi za Afya na Tiba katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Huu ni uamuzi wa msingi ambapo Zanzibar imepata uwezo wa kufundisha madaktari watakaotambulikana kupitia Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Utaratibu huu utaihakikishia Serikali kwamba mafunzo ya udaktari yanafundishwa kila mwaka na yanakuwa endelevu.

Katika hatua nyengine ya kukiimarisha Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya, chuo hicho nacho kinaunganishwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Lengo la Serikali ni kuongeza ufanisi na kuandaa wataalamu wa fani za afya katika kiwango cha shahada mbali mbali.

Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo inaendelea kuimarisha hospitali kuu ya Mnazi Mmoja kuifanyia upanuzi kwa kuongeza baadhi ya majengo, ili iweze kutoa huduma katika kiwango cha Hospitali ya Rufaa. Vile vile, Hospitali ya Abadalla Mzee ya Pemba inajengwa upya na kupatiwa vifaa vipya vya kisasa. Aidha, juhudi za kuzipandisha daraja Hospitali za "Cottage" za Makunduchi na Kivunge zimefikia hatua kubwa na kwa upande wa Micheweni na Vitongoji hatua zinaendelea. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikishajihisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika sekta ya afya jambo ambalo limekuwa likisaidia sana katika kuimarisha huduma za afya nchini.

Katika jitihada za kuimarisha maslahi na ustawi wa wafanyakazi, Serikali inaendelea kurekebisha Miundo ya Utumishi (Scheme of service) ya wafanyakazi wa sekta ya afya wakiwemo madaktari kwa lengo la kuhakikisha kuwa maslahi yao yanaongezeka ili kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi na kwa bidii zaidi.

Jengo jipya la kitengo cha maradhi ya Ubongo na Uti wa mgongo katika hospitali kuu ya Mnazi mmoja

Wanafunzi wa Chuo cha Taaluma ya Sayansi ya Afya Mbweni wakifanya majadiliano kuhusiana na masomo yao.

Mashine maalum ya kuchomea taka taka katika hospitali ya Kivunge

Sehemu ya kupokelea wagonjwa iliyopo katika jengo jipya la kupokelea wagonjwa katika hospitali ya Kivunge linalotarajiwa kuanza kazi mda si mrefu

Chumba cha matibabu ya meno kikiwa na mashine za kisasa katika hospitali ya Cotage Makunduchi

Sekta ya Utalii

Kuimarika kwa miundo mbinu Zanzibar imekuwa ni moja ya vichocheo vinavyosababisha idadi ya watalii kuendelea kuongezeka siku hadi siku na hivyo kufikia lengo la Serikali la kuifanya sekta hiyo kuwa sekta kiongozi katika uchumi wa Zanzibar.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Saba, iliingia madarakani ikiwa na dhamira kubwa ya kuiimarisha sekta ya utalii lengo likiwa ni kuibadilisha sura ya sekta hiyo ili iwe na mchango mkubwa zaidi katika uchumi kama sekta kiongozi kwa kuzingatia Mpango Mkuu wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA II)

Katika kutekeleza dhamira hiyo, tarehe 16 Oktoba, 2011 Serikali iliitangaza dhana ya 'Utalii kwa Wote' katika Mkutano wa Sita wa Baraza la

Mazingira ya hoteli za kitalii ukanda wa pwani ya Mashariki Zanzibar

Mazingira ya hoteli za kitalii katika kijiji cha Nungwi Kaskazini Unguja

Biashara la Zanzibar katika Hoteli ya Bwawani.

Kamati za Utalii kwa wote za Wilaya za Unguja na Pemba tayari zimeundwa ili kuziimarisha huduma za utalii kwenye Wilaya, na vile vile kuwahamasisha wananchi kuendeleza miradi ya uzalishaji mali, hususan kilimo cha mboga mboga, matunda, biashara ndogo ndogo na kadhalika ambazo wataziuza katika hoteli za kitalii.

Chuo cha Maendeleo ya Utalii kilichoko Maruhubi kinaimarishwa ili kitekeleze kwa ufanisi zaidi lengo la kujenga rasilmali watu wenye ujuzi, utaalamu na stadi zinazohitajika. Lengo la Serikali ni kukifanya chuo hicho kiendelee kutoa mafunzo ya utalii unaotilia maanani, mila, utamaduni na desturi zetu pamoja na hifadhi ya mazingira.

Hivi sasa Serikali imeshachukua hatua ya kuibua maeneo mapya ya vivutio vya utalii yakiwemo mapango, michezo ya asili, matamasha, maeneo ya hifadhi ya wanyama. Hatua zinachukuliwa za kuimarisha utalii wa kumbukumbu za kihistoria kwa maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba, kuimarisha utalii wa kiutamaduni na kuuendeleza

utalii wa ndani wenye kuyatunza mazingira.

Serikali imeamua kukiunganisha Chuo cha Maendeleo ya Utalii kwenye uongozi wa SUZA ili kitoe elimu ya juu kwenye fani ya Utalii.

Serikali inaendelea kushirikiana na taasisi binafsi ikiwemo Jumuiya ya ZATI na ZATO katika kuuimarisha utalii na kuitangaza Zanzibar kiutalii nje ya nchi kwa njia mbali mbali.

Hoteli za kisasa zinaendelea kujengwa na wawekezaji mbali mbali wa ndani na nje ya nchi. Vilevile hatua za kuzipanga hoteli katika madaraja yake zimeanza kuchukuliwa kwa lengo la kutambua ubora wa huduma na kuimarisha mapato ya Serikali.

Tokea kuanzisha mpango wa Utalii kwa Wote, mafanikio ya utalii yamezidi kuimarika. Idadi ya watalii wanaotembelea Zanzibar imekuwa ikiongezeka hadi kufikia watalii 181,301 mwaka 2013 ikilinganishwa watalii 169,223 waliotembelea mwaka 2012. Takwimu za mwaka 2014 zinaonesha idadi itaongeza zaidi kwani hadi Julai watalii wapatao 156,611 walikuwa wameshatembelea Zanzibar.

Sekta ya Umeme na Maji Safi na Salama

Ndoto za wananchi wa Zanzibar kuona kuwa tatizo la huduma ya umeme Zanzibar linaondoka zilianza kuyakinika baada ya kushuhudia kuwasili waya wa umeme kwenye bandari ya Malindi na kumuona Rais wa Zanzibar akiangalia waya huo Oktoba 5, 2012. Lakini furaha iliongezeka zaidi kwa wananchi wa Ukunjwi, Pemba na maeneo mengine ya Zanzibar baada ya huduma hiyo kufikishwa kwenye maeneo yao. Aidha, Ujenzi wa matangi ya maji na visima katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba kama inavyoonekana kwenye picha hizi ni jitihada za makusudi za Serikali kukabiliana na tatizo la maji Zanzibar kama ilivyoahidiwa kwenye Ilani ya CCM ya mwaka 2010 – 2015.

Nishati ya umeme ni muhimu katika kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea. Katika kuendeleza kazi za usambazaji wa nishati ya umeme na kukuza maendeleo ya kiuchumi na kijamii, Serikali imekamilisha utekelezaji wa kujenga njia ya pili ya umeme iliyopita chini ya bahari kutoka Ras Kiromoni Tanzania Bara hadi Fumba, Unguja. Serikali inaendelea na usambazaji umeme mjini na vijijini vikiwemo visiwa vidogo vidogo vinavyoishi watu katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba.

Uzinduzi wa Umeme katika kijiji cha Ukunjwi

Uzinduzi wa Mradi wa kusambaza umeme vijijini

MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA)

Uzinduzi wa Tangi la maji Ziwani Wilaya ya Chake chake

Katika kipindi cha miaka minne iliyopita, Mamlaka ya Maji Zanzibar imefanikiwa kutekeleza miradi mikubwa na program ambazo Mamlaka hiyo inaamini kuwa kukamilika kwake itakuwa imetekeleza kikamilifu Ilani ya CCM 2010 - 2015 na hivyo kwa kiasi kikubwa kuondoa tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama Unguja na Pemba.

Mradi wa maji wa Mkoa wa Mjini Magharibi uliotekelezwa chini ya ufadhili wa Serikali ya Japan pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, umeweza kutekelezwa kama ulivyopangwa ambapo utekelezaji wake unahusisha uchimbaji visima kumi na moja(11), ujenzi wa matangi manne (4) matangi mawili ya welezo, lenye uwezo wa kuhifadhi lita za ujazo milioni nne (lita 4,000,000) kwa kila moja , Tangi la Dole, tangi la Kinuni na kazi ya ufungaji wa mabomba makubwa yenye urefu wa kilomita 41.4.

Mradi wa Usambazaji wa maji na usafi wa Mazingira nao umetekelezwa kwa mafanikio makubwa ukihusisha uchimbaji wa visima 41 vya uzalishaji, ujenzi wa matangi ya kuhifadhia maji (17) katika miji ya Chake Chake, Wete na Mkoani, Nungwi, Matemwe, Machui na Dunga - Tunguu kwa Unguja na Wambaa, Mizingani, Ndagoni, Vitongoji na Kambini - Mchangamdogo kwa Pemba.

Kazi za ulazaji wa mabomba makubwa yanayotoka visimani kuelekea kwenye matangi na kutoka kwenye matangi kwenda kwa watumiaji pia zimefanyika kwa mafanikio makubwa. Ujenzi wa matangi ya uvunaji maji ya mvua maskulini, ujenzi wa vyoo sabini na tisa (79) katika skuli za Unguja na Pemba umefanyika.

Mradi wa kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji ambao unatekelezwa kwa ufadhili wa Serikali ya Japan kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, umetekeleza kazi zake kwa kuwajengea uwezo watendaji wa Mamlaka hiyo ili waweze kumudu majukumu yao ipasavyo.

Mradi wa uchimbaji wa visima Khamsini 50 wa Ras Al Khaimah unaofadhiliwa na Mtawala wa Rasa-al-Khaimah tayari umekamilisha uchimbaji wa visima 38 katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

Mradi wa maji safi na salama wa afya na mazingira (AAP) umetekelezwa kwa kushirikiana kwa pamoja kati ya wananchi wa Nungwi kupitia Kamati ya mazingira, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Ofisi ya Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kupitia Idara ya Mazingira.

Tangi jipya la Kusambaza maji kijiji cha Machui na vyengine vya jirani

Sekta ya Miundombinu na Mawasiliano



Kazi za ujenzi wa miundombinu ya barabara Unguja na Pemba zimepewa kipaumbele maalum kutokana na umuhimu wake katika kukuza uchumi wa Taifa pamoja na kustawisha maisha ya jamii ya Wazanzibari. Pongezi za pekee zinaelekezwa kwa Serikali ya Marekani kupitia Mfuko wa Changamoto za Millenia kwa kuunga mkono jitihada za Serikali katika kufanikisha mradi wa ujenzi wa barabara tano Kisiwani Pemba. Aidha, Uimarishaji wa bandari na uwanja wa ndege ili uwe wa kisasa yalikuwa ni malengo mengine ya serikali ambayo kama inavyoonekana kwenye picha, Dk. Shein amekuwa kwa muda wote akifuatilia kwa karibu utekelezaji wake.

Kazi za ujenzi wa miundombinu ya barabara Unguja na Pemba zimepewa kipaumbele maalum kutokana na umuhimu wake katika kukuza uchumi wa Taifa pamoja na kustawisha maisha ya jamii ya Wazanzibari.

Wakati uongozi wa Awamu ya Saba ulipoingia madarakani, kazi ya kwanza ilikuwa kuendeleza kazi iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika maeneo mbalimbali likiwemo la miundombinu ya kiuchumi.

Kwa upande wa barabara za Unguja, uongozi wa Awamu ya Saba umekamilisha ujenzi wa barabara ya Mfenesini – Bumbwini yenye urefu wa kilomita13 na barabara ya Welezo – Dunga yenye kilomita 12.75 kwa kiwango cha lami.

Aidha, kwa upande wa Pemba barabara zenye urefu wa (km44.7) kupitia mradi wa NORAD zimekamilika ambazo ni barabara za Mtambile–Kengeja–Mwambe (km9), Kenya–Chambani (km3.2), Mizingani–Wambaa (km 10), Chanjamjawiri– Tundauwa (km 10), Chanjaani– Pujini (km 5) na Mtambile – Kangani (km 6.2).

Barabara nyengine zenye urefu wa (km 35) kupitia mradi wa MCC ambazo ni Bahanasa–Daya–Mtambwe (km 13.6), Mzambarau Takao–Pandani Finya (km 8),

Uzinduzi wa barabara S Mkoa wa Kaskazini Pemba

Uzinduzi wa barabara ya Amani Mjini Unguja

Mzambaraukarim-Mapofu (km 8.6), Chwale-Kojani (km 2) na Kipangani -Kangagani (km 3) zimekamilishwa kwa kiwango cha lami katika miaka minne ya Uongozi wa Awamu ya saba.

Ziko barabara ambazo ujenzi wake unaendelea lakini unatarajiwa kukamilika ndani ya Awamu hii ambazo kwa upande wa Unguja ni Jendele-Cheju-Kaebona (km 11.7) na Koani-Jumbi (km 6.3) na kwa upande wa Pemba ni barabara za Wete - Konde (km 15) na Wete-Gando (km 15) ambazo Mkandarasi ameahidi kukamilisha kazi mwezi Disemba 2014.

Kwa upande wa barabara ya Chakechake hadi Wete yenye kilomita 21, matayarisho ya kupata mkopo kutoka Saudi Fund yanaendelea na mara tu taratibu zitakapokamilika ujenzi utaanza mara moja.

Aidha, Uimarishaji wa bandari na uwanja wa ndege ili uwe wa kisasa yalikuwa ni malengo mengine ya serikali ambayo kama inavyoonekana kwenye picha, Dk. Shein amekuwa kwa muda wote akifuatilia kwa karibu utekelezaji wake.

Uzinduzi wa barabara tano (5) za mkoa wa Kaskazini Pemba

Uzinduzi wa barabara ya Mfenesini

Uzinduzi wa barabara Mkoa wa Kusini Pemba

Uzinduzi wa barabara S Mkoa wa Kaskazini Pemba

Uzinduzi wa bandari ya Malindi tarehe 8 Julai 2013

Kutokana na kutambua kuwa huduma za bandari zinao mchango mkubwa katika kukuza uchumi na ustawi wa jamii, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imejenga majengo mapya katika bandari ya Malindi, pamoja na matengenezo ya maeneo ya kuhifadhia makontena bandarini

Uzinduzi wa sehemu ya abiria katika bandari ya Malindi

Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume baada ya matengenezo makubwa

Maendeleo endelevu ya uchumi yanategemea sana ubora wa miundombinu ya kiuchumi ambayo hujumuisha barabara, bandari, viwanja vya ndege na umeme. Katika kipindi cha miaka minne iliyopita, Serikali imeendelea kukamilisha ujenzi wa barabara kadhaa za Unguja na Pemba pamoja na kuendeleza ujenzi wa uwanja wa ndege wa kisasa.

Ziara ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume

Zao la Karafuu

Magunia ya Karafuu tayari kwa kusafirishwa

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizindua msimu wa karafuu kwa mwaka 2014/15 katika sherehe zilizofanyika kwenye ghala la karafuu Wilaya ya Mkoani Mkoa wa Kusini Pemba tarehe 09 Julai, 2014.

Tumeweza kurejesha hadhi ya zao la karafuu kwa kuliimarisha Shirika la Biashara la Taifa. Ufuatiliaji mzuri na wa karibu wa zao la karafuu umelifanya zao hilo kuimarika zaidi katika kipindi cha miaka minne kuliko miaka iliyopita.

Tokea ZSTC lianze kutekeleza mageuzi mnamo mwaka 2011/2012, tija kubwa imepatikana kwa wananchi wenye mashamba ya mikarafuu ambao wamenufaika moja kwa moja kutokana na mauzo ya karafuu na wasiomiliki ambao wamenufaika kutokana na mzunguko wa fedha za mauzo ya karafuu.

Sekta ya Habari na Utamaduni

Jengo la Sauti ya Tanzania Zanzibar ambalo limefanyiwa matengenezo makubwa na kuwa studio mpya na ya kisasa kwa lengo la kutoa fursa kwa wasanii kurikodi na kuhifadhi kazi zao za sanaa na kuendeleza tasnia ya utamaduni wa nchi yetu

Habari ni nyenzo muhimu katika kujenga misingi imara ya maendeleo kutokana na ukweli kwamba maendeleo yanaweza kupatikana iwapo tu kunaweko na upatikanaji wa taarifa kutoka sehemu tofauti. Kwa msingi huo, habari zina umuhimu wa pekee katika ujenzi wa maendeleo endelevu kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu cha 18 (2) kinaeleza, “Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbali mbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi, na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii”.

Kwa kutambua wajibu huo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba imechukua juhudi maalum zenye lengo la kukuza na kuendeleza

Tamasha la Utamaduni la Urithi wa Mangapwani Wilaya ya Kaskazini B Unguja

uhuru wa vyombo vya habari ili hatimaye viweze kutekeleza jukumu lake kwa ufanisi na kufikia lengo lililowekwa.

Ndani ya kipindi hiki cha miaka minne, Serikali imetekeleza mambo mengi makubwa ya kuimarisha na kuiendeleza sekta ya habari nchini. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na kuweza kwenda sambamba na mabadiliko ya kimataifa ya utangazaji kutoka mfumo wa utangazaji wa analogi kwenda dijitali kwa kuweza kuwahi muda wa kuhama kutoka kwenye analogi kwenda kwenye digitali ndani ya muda uliowekwa na Jumuiya ya Mawasiliano ya Afrika ya Mashariki (East Africa Communication Organization) wa Desemba 31, 2012 licha ya gharama kubwa ya fedha zilizotumika kununua vifaa vya kisasa kufanikisha lengo hilo.

Vifaa vilivyonunuliwa ni vya miundo mbinu kamili ya dijitali ambavyo vimeigharimu Serikali kiasi ya dola 4,342.737 na vya studio za Televisheni za Karume House Unguja na Mkoroshoni Pemba dola 1,062,138.09.

Hatua hiyo ya kuweka vifaa vya dijitali imewanufaisha wananchi kwa kupata huduma mpya za matangazo hayo.

Zaidi ya shilingi 1,496,600,000 zimetumika kwa kazi ya matengenezo ya mnara wa mawimbi mafupi (short wave) hatua ambayo imewezesha matangazo yanayorushwa na kituo kilichoko Dole yanasikika

Ziara ya waandishi wa habari kwenye miradi ya utalii

hadi Mashariki ya Mbali. Kwa hiyo matakwa ya ilani ya uchaguzi ya CCM imetekelezwa kikamilifu.

Shirika la Magazeti ya Serikali katika kipindi cha miaka minne limeweza kuongeza maeneo ya usambazaji wa magazeti katika vijiji vya Mkokotoni, Nungwi, Uroa, Makunduchi, Jambiani kwa Unguja. Kwa upande wa Pemba maeneo yaliongezeka ni Madenjani, Wete, Konde.

Shirika hilo limeweza kutimiza lengo hilo katika Mkoa wa Dar es Salaam na Mikoa mingine ya Tanzania Bara ikiwemo Tanga, Iringa, Shinyanga, Tabora, Mbeya, Bukoba, Morogoro, Mtwara, Kigoma, Arusha, Mwanza, Songea, Singida na Dodoma ili kuweza kulitafutia soko zaidi.

Chuo cha Uandishi wa Habari kimeimarishwa kwa kupatiwa vifaa vya kufundishia pamoja na kuajiriwa walimu wenye ujuzi. Hatua hiyo imekifanya chuo hicho hivi sasa kutoa mafunzo ngazi ya stashahada badala ya cheti yaliyokuwa yakitolewa mwanzo. Kiwango cha idadi ya wanafunzi nacho kimeongezeka kutoka 75 ya mwaka 2009/2010 hadi kufikia 146 kwa mwaka 2013/2014.

Harakati za Kinamama katika jamii

Utu, uungwana na unyenyekevu wa Mke wa Rais wa Zanzibar Mama Mwanamwema Shein na Mke wa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar Mama Asha Suleiman Iddi ambao wamekuwa wakiwaonesha wananchi wa Zanzibar katika kipindi cha miaka minne sasa kwa kukutana, kuwasaidia na kuwafariji wazee na watu wenye kuishi katika mazingira magumu kama inavyoonekana kwenye picha mbali mbali vimewajengea heshima kubwa kwa wananchi wa Zanzibar.

Wakati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akitimiza miaka minne ya uongozi wake kuiongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa kitaifa kwa ufanisi mkubwa, harakati za mchango wa mama Mwanamwema Shein pamoja na mke wa Makamo wa Pili wa Rais Mama Asha Suleiman Iddi katika kusaidia vikundi vya kijamii umeonekana kutoa msukumo mkubwa katika kuviwezesha vikundi hivyo kujenga misingi ya kupambana na umasikini.

Ziara ya Mama Mwanamwema Shein na Mama Asha Suleiman Mkoa wa Kusini Pemba tarehe 19 Disemba 2013

Kazi iliyofanywa na mama Mwanamwema Shein kwa kushirikiana na Mama Asha Suleiman Iddi pamoja na wake wengine wa viongozi wa Chama cha Mapinduzi katika kipindi cha miaka minne ya kusaidia maendeleo ya kijamii mjini na vijijini inastahili kupongezwa kwani imekuwa ikivihamasisha vikundi vya kijamii vikiwemo vya akinamama, wazee na makundi maalum kujiimarisha kiuchumi katika makundi yao.

Miongoni mwa ziara walizozifanya katika kipindi hiki cha miaka minne ya uongozi wa Dk. Shein ni

Mama Mwanamwema Shein akikabidhi msaada wa mabati katika Skuli ya Fujoni

kutembelea vikundi vya ushirika vya akinama katika vijiji vya Ukongoroni, Charawe, Nungwi, Tazari na Ushirika wa Mbweni, ambapo walikabidhi vifaa mbali mbali pamoja na fedha taslimu zenye jumla ya Tsh. 2,683,750. Aidha, mama Shein katika ziara zake hizo walikabidhi vifaa mbali mbali vikiwemo vyarahani, mabero, mikasi, vizoleo, tepu, reki, mapanga na vifaa nyengine vya kufanyia kazi.

Walipotembelea ushirika wa Mbweni mama Mwanamwema alikabidhi Tsh. 2,000,000 kwa ushirika huo kwa lengo la kuuendeleza.

Ziara ya Mama Mwanamwema Shein na Mama Asha Suleiman Mkoa wa Kaskazini Unguja tarehe 8 Mei 2013

Katika sherehe za makabidhiano ya fedha hizo kulifanyika harambee ya kuuchangia ushirika huo ambapo Tsh. 5,864,000 zilipatikana na kufanya idadi ya fedha zote zilizopatikana kufikia Tsh. 7,864,000.

Miongoni mwa shughuli nyengine muhimu alizozifanya mama Mwanamwema Shein akifuatana na mke wa Makamo wa Pili wa Rais mama Asha Suleiman Iddi na wake wa Wabunge na Wawakilishi wa C.C.M akiwemo mke wa Balozi wa China mama Wu Yan ni ziara ya kuvitembelea vikundi mbali mbali vya ushirika kisiwani Pemba.

Ziara ya Mama Mwanamwema Shein na Mama Asha Suleiman Mkoa wa Kaskazini Unguja tarehe 8 Mei 2013

Kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba vikundi vilivyofaidika na misaada hiyo ni Kikundi cha Ushirika cha Tupendane, kinachojishughulisha na shughuli za ushoni wa nguo na ufumaji wa mashuka, Kikundi chengine ni cha Alla Atosha, wanaojishughulisha na kilimo cha migomba, ufumaji na saloon, kikundi cha Nia njema kinachojishughulisha na utengenezaji wa nguo za batiki na kikundi chengine cha Tuhamasike, kinachojishughulisha na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na kazi za ufinyanzi wa vyungu na mikungu.

Mama Mwanamwema aliwataka wananchi wa vijiji hivyo kufikiria zaidi hatua za kuanzisha miradi ya maendeleo badala ya kupoteza muda mwingi kusikiliza propaganda za baadhi ya watu wasioitakia mema Zanzibar ambao wamekuwa wakisambaza taarifa zisizokuwa za ukweli kupitia mitandao ya kijamii zenye lengo la kuchafua hadhi na heshima ya vijiji vyao.

Ziara za Dk. Shein nje ya nchi

Ziara ya Dk. Shein nchini Uturuki tarehe 28 Machi 2011

Tokea kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Zanzibar ma Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi miaka minne iliyopita, Dk. Ali Mohamed Shein amekuwa akifanya ziara katika nchi mbali mbali za nje kwa lengo la kuimarisha uhusiano baina ya nchi alizozitembelea na Tanzania na hasa Zanzibar, na kutafuta fursa zitakazosaidia kuimarisha uchumi wa nchi hizo kwa kuanzisha miradi ya uwekezaji kwa maslahi ya pande zote husika.

Ziara ya kwanza ya Dk. Shein nchi za nje baada ya kuapishwa kuwa Rais wa Zanzibar ilikuwa ni ziara nchini Uturuki iliyofanyika kuanzia tarehe 28 Aprili, 2011 hadi tarehe 2 Mei, 2011. Pamoja na mambo mengine ziara hiyo ilikuwa na madhumini ya kuimarisha uhusiano uliyopo baina ya Uturuki na Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla na kuendeleza ushirikiano katika nyanja za siasa, Uchumi na Biashara, Elimu na Afya. Maeneo mengine ni Miundombinu na Ujenzi, Kilimo, Uvuvi, Utalii, Utamaduni na Uwekezaji.

Ziara ya Dk. Shein nchini Ras Al - Khaimah tarehe 12 Novemba 2011

Katika ziara hiyo pande hizo zilikubaliana mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na Uturuki kusaidia kukiimarisha Chuo cha Kilimo Kizimbani ili kiweze kutoa wataalamu hadi kufikia kiwango cha stashahada, kuanzisha ushirikiano wa kimasomo baina ya Uturuki na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na kushirikiana katika kuendesha biashara ya utalii.

Katika mazungumzo baina ya pande hizo mbili, ilikubalika kwamba Bunge la Uturuki na Baraza la Wawakilishi Zanzibar yaanzishe uhusiano rasmi wa kikazi, na kwa upande wa sekta ya afya, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaandaa utaratibu wa kuwapeleka wataalamu wa Afya nchini Uturuki kujifunza masuala ya utafiti wa dawa na tiba.

Ziara nyengine ambazo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amezifanya ni ziara katika Umoja wa Falme za nchi za Kiarabu Ras Al-Khaimah katika mwezi wa Novemba, 2011 na nchini China na Vietnam mwezi Juni, 2013. Nchini Vietnam na China ilikubaliwa kwamba nchi



Ziara ya Dk. Shein nchini China tarehe 28 Mei 2013

hizo zitashirikiana na Zanzibar katika kuimarisha sekta ya kilimo na uvuvi kwa kuzingatia uzoefu na utaalamu uliopo kwenye nchi hizo.

Nchi nyengine ni Uholanzi ambayo ziara ilifanyika mwishoni mwa mwezi wa Agosti hadi mwanzoni mwa mwezi Septemba 2013 ambako kama zilivyo nchi nyengine alikutana na wafanyabiashara wanaomiliki makampuni makubwa, ambapo mazungumzo yalihusisha uwezekano wa wafanyabiashara hao kuja kuwekeza Zanzibar. Miezi michache baadae wafanyabiashara hao wakiongozwa na Waziri wa Biashara za Nje wa Nchi hiyo Bibi Liliane Ploumen walifika Zanzibar ili kujionea wenyewe mandhari ya Zanzibar na fursa za kuwekeza.

Dk. Ali Mohamed Shein vile vile alitembelea nchini India ambako yeye na ujumbe aliofuatana

Ziara ya Dk. Shein nchini Vietnam tarehe 23 Novemba 2012

nao walifikia makubaliano kadhaa ikiwa ni pamoja na India kusaidia jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuleta Mapinduzi ya Kilimo, ujenzi wa Chuo cha amali cha akinamama na kuialika kampuni ya Mahindra & Mahindra ili kuangalia uwezekano wa kampuni hiyo kunzisha biashara zake Zanzibar.

Mwamzoni mwa mwezi Septemba 2014, Rais wa Zanzibar alihudhuria mkutano wa tatu wa kimataifa wa nchi za visiwa uliofanyika nchini Samoa kabla ya kwenda visiwa vya Comoro tarehe 15 Juni 2013, kwa mwaliko wa Rais wa nchi hiyo Dk. Ikililou Dhoinine.

Funzo lililopatikana kutokana na ziara mbali mbali za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nchi za nje ni kwamba uimara

Ziara ya Dk. Shein nchini Uholanzi tarehe 27 Agosti 2013

wa kisiasa, amani na utulivu kwa jumla ni muhimu katika kuwavutia wawekezaji kuja Zanzibar kuliko sehemu nyengine ya Afrika na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo.

Historia ya visiwa vya Zanzibar na nafasi yake kijiogorafia ni kivutio kikubwa cha utalii na wawekezaji kutoka nchi za nje. Fursa ya kupanua biashara mbali mbali ikiwemo utalii, bidhaa za kilimo, vifaa vya kilimo, vyakula na kadhalika ni kubwa iwapo juhudi za makusudi zitachukuliwa kujitangaza katika nchi mbali mbali duniani.

Ziara ya Dk. Shein nchini India tarehe 1 Februari 2014

Ziara ya Dk. Shein nchini Comoro tarehe 15 Septemba 2014

Ziara ya Dk. Shein nchini Samoa tarehe 1 Septemba 2014

Uhifadhi wa Mazingira, Dawa za Kulevya na Ukimwi

Hali halisi katika soko la mboga Mombasa

Mazingira ni suala mtambuka ambalo linagusa sekta zote za kiuchumi na kijamii. Ni dhariri kwamba uharibifu wa mazingira ni tishio la taifa zima na mazingira endelevu ni muhimu kwa maslahi ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo. Katika kuendeleza suala la uhifadhi wa mazingira, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya wamu ya saba, pamoja na mambo mengine, suala hilo linashughulikiwa na Ofisi ya Makamo wa kwanza wa Rais.

Aidha, Ofisi hii imepewa jukumu la kusimamia, kuratibu na kuhakikisha kuwa jamii ya Zanzibar inaishi katika mazingira endelevu bila ya athari za Ukimwi, VVU, dawa za kulevya na inavyolinda haki na fursa za watu wenye ulemavu.

Uongozi wa Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais umekuwa ukishiriki kikamilifu katika utekelezaji wa malengo ya ofisi hiyo. Miongoni mwa matukio muhimu yaliyoshuhudiwa ndani ya ofisi hiyo ni pamoja na Kampeni ya Uhifadhi Mazingira, Uanzishwaji wa Mfuko wa Walemavu pamoja na Uzinduzi wa Sera ya Mazingira

Kama zilivyo Wizara nyengine za Serikali, Ofisi ya Makamo wa kwanza wa Rais imeripoti mafanikio makubwa katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.

Miongoni mwa mambo ambayo Serikali imeelekezwa na Ilani ya CCM 2010 - 2015 kuyafanya katika suala zima la mazingira, na ambayo yametekelezwa kwa ufanisi mkubwa ni pamoja na kuandaa sera ya mazingira na kusimamia utekelezaji

Uzinduzi wa mkakati wa Tabianchi

wa mpango wa Hifadhi ya Mazingira katika maeneo ya ardhi, bahari na ukanda wa pwani.

Vile vile suala la kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa utunzaji na uhifadhi wa mazingira katika maeneo ya makazi na sehemu za kazi, viwanda na mahoteli nalo limesimamiwa ipasavyo katika kipindi hiki cha miaka minne.

Jitihada za kuimarisha zoezi la kitaifa la kupanda miti na miti ya asili kila mwaka katika maeneo mbali mbali yakiwemo waliyotengwa maalum kwa ajili hiyo zimechukuliwa na Serikali ambapo viongozi wa vitongoji, vijiji na mitaa wamekuwa wakipita mara kwa mara kukagua miti iliyoapandwa ili kuhakikisha kuwa miti hiyo inastawi.

Kuhusu jitihada za matumizi ya dawa za kulevya, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais imeweza kuandaa mkakati wa uingizaji na utumiaji wa madawa ya kulevya kwa kuwashirikisha masheha pamoja na polisi jamii. Hatua hiyo inatazamiwa kuleta mafanikio makubwa katika kupunguza matumizi ya dawa hizo kwa vile jamii itakuwa imeshirikishwa kikamilifu katika utekelezaji wa mpango huo.

Aidha, Ofisi hii imeweza kufanya tafiti moja

Athari za kimazingira katika kijiji cha Fungurefu, Mkokotoni

kwa ajili ya watu wenye ulemavu ili kujua mahitaji yao muhimu katika maisha yao ya kila siku. Utafiti huo pia umezingatia jinsi gani watu wenye ulemavu wanaweza kufikiwa kwa urahisi na namna ya kuwapatia haki yao ya elimu kwa kuzingatia ulemavu walionao na nanma ya kuweza kuwawekea mazingira rafiki kulingana na hali zao.

Ofisi ya Makamo wa kwanza wa Rais imeweza kuanzisha mfuko wa Watu Wenye Ulemavu pamoja na bodi mpya ya Tume ya Ukimwi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi zake.

Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imetenga fungu maalum kwa ajili ya kuzisaidia nyumba za kurekebisha tabia "SOBER HOUSE" kwa vijana walioamua kuacha matumizi ya dawa za kulevya.

Sambamba na hatua hiyo, Serikali imeweka eneo maalum kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya karekebisha tabia. Eneo hilo liko KIDIMNI katika Wilaya ya Kati Unguja.

Madawa ya kulevya pamoja na maambukizi ya VVU ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazowakabili vijana wa Zanzibar. Dawa za kulevya zimekuwa zikiathiri afya za watumiaji ambao wengi wao ni vijana na hudhoofisha nguvu kazi na uchumi wa Taifa.

Aidha, upo uhusiano mkubwa kati ya matumizi ya dawa hizo na maambukizi ya VVU.

Ili kuendeleza mapambano dhidi ya dawa za kulevya na kudhibiti maambukizi ya VVU, Serikali imekuwa ikisimamia hatua mbali mbali zenye lengo la kupunguza au kuondoa kabisa tatizo hilo.

Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kuendeleza kushirikiana na asasi za kijamii katika kuhamasisha na kuelimisha vijana athari za dawa za kulevya ni kuwashawishi waachane na matumizi ya dawa hizo.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na mkewe Mama Mwanamwema Shein walipata fursa ya kuwatembelea vijana waliokuwa wameathirika na dawa za kulevya na ambao wako kwenye nyumba maalum za kurekebisha tabia za vijana huko " Sober house" iliyoko Limbani wete.

TASAF, CDF na Kero za Muungano zimeratibiwa ipasavyo

Makamo wa Pili wa Rais akizungumza na wananchi wa kijiji cha Donge

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kupitia Idara na Tasisi zake katika kipindi cha miaka minne (2010–2014) imepata mafanikio makubwa ya kiutendaji. Ofisi imefanikiwa kusimamia na kuratibu miradi midogo midogo ya wananchi kwa kupitia mpango wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF II na III) na mfuko

Shughuli za ukaguaji wa miradi ya maendeleo kwenye maeneo mbali mbali Unguja na Pemba, kuonana na Wananchi kuzungumzia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Serikali pamoja na changamoto zake, kama inavyoonekana pichani zimekuwa kazi za msingi ambazo zimekuwa zikifanywa na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais katika kipindi cha miaka minne iliyopita

Uzinduzi wa Kiwanda kipya cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali Maruhubi Zanzibar tarehe 28 Disemba 2013

wa maendeleo ya jimbo (CDF) kwa lengo la Serikali kuwasaidia wananchi wake kupunguza umaskini. Katika Utekelezaji wa TASAF awamu ya III, zaidi ya kaya 6,000 zinanufaika na mpango huo kwa Unguja na Pemba. Kwa upande wa mfuko wa maendeleo ya Jimbo jumla ya majimbo 50 Unguja na Pemba yamepatiwa fedha kwa awamu tatu.

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imefuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (CCM) ya mwaka 2010–2015 katika Wizara zote za SMZ na kuandaa taarifa ya utekelezaji wa Ilani hiyo kwa kipindi cha miaka miwili (2010–2012). Aidha, Ofisi inaendelea na maandalizi ya taarifa ya utekelezaji wa ilani kwa kipindi cha miaka mitano (2010 - 2015).

Ofisi imeendelea kuratibu vikao vya kero za Muungano kati ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais kwa uongozi wa mwenyekiti Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia kuratibu vikao vya mashirikiano kati ya SMT na SMZ.

Ofisi imeandaa sera ya kukabiliana na maafa ya mwaka 2013, Mkakati wa mawasiliano wakati wa maafa na mpango wa kujikinga na kukabiliana na maafa, ngazi ya Wilaya. Aidha, Ofisi imeandaa muongozo wa ufatiliaji na tathmini wa sera ya maafa.

Ofisi kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Tanzania ,Mashirika ya Kimataifa na Taasisi zisizokuwa na Serikali ilisimamia na kuratibu uokoaji wahanga wa ajali mbili kubwa za Meli MV Spice Islander 1 iliyotokea Oktoba 2011 na MV Skagit iliyotokea Julai 2012 na kusimamia na kuratibu michango ya fedha kwa waathirika wa maafa hayo .

Ofisi imeimarisha shughuli za upigaji chapa kwa kufanya matengenezo makubwa ya jengo jipya la kiwanda cha uchapishaji Maruhubi na kununua na kufunga mashine mpya za kisasa za digitali. Kiwanda tayari kimehamia maruhubi na tayari kimeanza kufanya kazi.

Ofisi imesimamia na kuratibu ufunguzi wa ofisi ya COSTECH Zanzibar. Aidha COSTECH inaharamia masomo katika ngazi ya shahada ya pili fani ya utafiti kwa wanafunzi 13 wa Zanzibar

Malipo ya fidia kwa wananchi wa Tumbatu

Ofisi imesimamia kwa ufanisi mkubwa maadhimisho ya sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambazo zilikuwa za kipekee na aina yake. Maadhimisho hayo yalijumuisha Maonyesho, Michezo, Fensi na siku ya kilele ya maadhimisho hayo. Aidha, Ofisi kwa kushirikiana na ofisi ya Waziri Mkuu imeratibu maadhimisho ya miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar .

Katika kipindi hiki cha miaka minne, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Baraza la Wawakilishi imepitisha kiasi ya miswada 36 ya sheria na jumla ya maswali 873 yaliulizwa na kujibiwa. Baraza la Wawakilishi Zanzibar kupitia njia mbali mbali limekuza mashirikiano na mahusiano na Mabunge mengine Duniani.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Tume ya Uchaguzi Zanzibar iliendesha chaguzi ndogo tatu (3) za Kidemokrasia katika majimbo ya Kiembesamaki, Uzini na Bububu. Vile vile, Tume ilifanya uchaguzi mdogo wa wadi ya Kiboje Wilaya ya kati. Katika chaguzi hizo wagombea wa Chama Cha Mapinduzi walipata ushindi. Tume ya uchaguzi imeliimarisha daftari la kudumu la Wapiga Kura .

Makamo wa Pili wa Rais na wanafunzi wa madrasa katika kijiji cha Makunduchi

Sekta ya Wafanyakazi na Wajasiriamali

Maslahi na motisha kwa wafanyakazi ni mambo yaliyopewa msukumo maalum na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba inayoongozwa na Dk. Ali Mohamed Shein kama inavyoonekana pichani ambapo ndugu Khamis Mikidadi anakabidhiwa zawadi ya Tsh. 500,000 taslim kutokana na utumishi wake ulitukuka kwenye sekta ya umma.

Kwa kujua kuwa wafanyakazi ni rasilimali watu na ndio msingi wa mageuzi yote ya kiuchumi na kijamii, Serikali imeweza kuimarisha mazingira bora ya kazi pamoja na kuongeza mara mbili kima cha chini cha mishahara ya watumishi wa umma kutoka Tsh 100,000 – 125,000 mwaka 2011/12. na Tsh 125,000 – 150,000 mwaka 2013/14. Aidha, katika mwaka 2013/14 SMZ ilifanya mazingatio maalum kwa watumishi wenye uzoefu usiopungua miaka 15 ya kazi na ambao ngazi yao ya elimu havizidi ngazi ya cheti. Wafanyakazi hao wameengezwa wastani wa Tsh 75,000 kutoka 150,000 – 225,000.hatua ambayo haijawahi kufanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tokea Mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964.

Kwa kutambua kwamba wananchi waliowengi bado ni masikini na wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa maarifa, ujuzi na mitaji katika kilimo, biashara na ujasiriamali hali ambayo ni kizuizi cha maisha bora na mapambano dhidi ya umasikini, tumeendeleza mafunzo na elimu ya ujasiriamali sambamba na kuimarisha mfuko wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kwa lengo la kukuza uwezo wake wa kutoa mikopo kwa wananchi walio wengi zaidi. Aidha, Serikali itaendelea kuunga mkono uundwaji wa vikundi vya SACCOS.

Kiwanda cha kukaushia Embe Cheju

Miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar

Maadhimisho ya sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar tarehe 12 Januari, 2014

Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari 1964, ndio tukio kubwa na muhimu la kihistoria kwa visiwa vya Zanzibar. Tukio hilo ndilo lililowakomboa Wazanzibari wote kutoka katika makucha ya ukoloni na kujenga mazingira muafaka ya Zanzibar huru kuungana na Tanganyika huru. Katika kipindi cha miaka minne iliyopita, Serikali imeendelea kuyalinda Mapinduzi hayo ikiwa ndio msingi wa maendeleo kamili, uhuru, haki, usawa wa binadamu na heshima ya kweli ya Wazanzibari.

Miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao ni wa kipekee katika Bara la Afrika umefikia miaka 50 tokea kuasisiwa kwake hapo tarehe 26, Aprili 1964. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa katika kipindi cha miaka minne iliyopita, imeendelea kuhakikisha kuwa Muungano huo unazidi kuimarika pamoja na kujenga mazingira endelevu ya kuimarisha fursa za kiuchumi miongoni mwa wananchi wa kila upande kwa lengo la kuwataka waone na kuamini kwamba Muungano huo sio tu ni ngao madhubuti ya umoja, amani na mshikamano wao, lakini pia ni daraja lisilotetereka la kuwafikisha katika azma yao ya kuondokana na umasikini na kuharakisha maendeleo ya Taifa kwa jumla

Maadhimisho ya sherehe ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kutima miaka 50 tarehe 26 Aprili, 2014

Sekta ya Ufugaji na Uvuvi

Wananchi wa Zanzibar wavuvi na wafugaji wamethibitisha kuwa mapinduzi katika sekta hizo yameweza kuwaletea tija zaidi kuliko ambavyo walikuwa wamezowea miaka iliyopita. Hii imethibitishwa na wafugaji wenyewe wakati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipowatembelea kwenye maeneo yao ya kazi Unguja na Pemba.

Ili kuleta Mapinduzi ya ufugaji, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa CCM imeendelea kuimarisha ufugaji wa kisasa wa ng'ombe wa maziwa, mbuzi na kuku wa nyama na mayai kwa lengo la kuongeza tija na kipato cha wafugaji.

Katika kipindi hiki cha miaka minne Serikali imeendeleza juhudi za kuwaendeleza wafugaji kupitia programu mbali mbali ikiwemo programu ya

Mabwawa ya kufugia samaki

kuimarisha huduma za mifugo (ASDP–L). Zaidi ya vikundi 335 vya Unguja na Pemba vilipewa mafunzo. Wafugaji wapatao 3,200 walitembelewa na kupewa ushauri. Vile vile, huduma za utafiti na utibabu wa wanyama ziliimarishwa na matengenezo ya Maabara ya Maruhubi na Chake Chake yalifanyika.

Kwa kuzingatia maumbile na jiografia ya Zanzibar, uvuvi ni shughuli muhimu ya kiuchumi miongoni mwa wananchi wa Zanzibar wanaoishi pembezoni mwa mwambao wa bahari. Serikali imeendelea kuwahamasisha wavuvi juu ya uanzishwaji wa vikundi vya ushirika na matumizi ya maarifa ya kisasa ili uvuvi wao uwe wa kisasa zaidi unaokidhi mahitaji ya soko la ndani.

Sekta ya Michezo

Dhamira ya dhati ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein katika kuimarisha sekta ya michezo nchini imedhihirika ndani ya miaka minne toka kuundwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa kwa ushiriki wake katika matukio tofauti ya michezo kama inavyoonekana pichani

Sera ya michezo inahimiza suala la ujengaji na uendelezaji wa viwanja vya kisasa kwa ajili ya michezo mbalimbali ikiwemo ya ndani. Katika kuhakikisha kuwa azma hiyo inatekelezwa, Serikali imechukua juhudi kubwa za kukuza tasnia ya michezo na hasa mpira wa miguu.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amekuwa akichukua juhudi maalum kufikia lengo hilo kwa kukutana na wanamichezo maarufu wastaafu ili

Dk. Shein akikabidhi kifimbo cha Malkia – Ikulu

kubadilishana nao mawazo juu ya namna bora zaidi ya kuirejeshea Zanzibar umaarufu wake katika medali ya michezo.

Miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyopatikana kimichezo katika kipindi hiki cha miaka minne ni pamoja na kuifanyia mapitio será ya michezo ili iendane na mazingira halisi ya sasa.

Aidha, Baada ya kubaini kuwepo kwa malalamiko mengi kutoka kwa wanamichezo wa mpira wa miguu juu ya hali mbaya ya uwanja wa kuchezea wa Amani, Serikali iliamua kukabiliana na hali hiyo, ambapo imelazimika kuchukua hatua za dharura za kuirejesha sehemu hiyo ya kuchezea katika kiwango kinachohitajika.

Hatua hiyo iliokuwa ni ya kuweka nyasi bandia katika uwanja huo wa Amani ili uendane na viwango vya Kimataifa. Zaidi ya shilingi 500,000,000/= zimetumika kwa kazi hiyo. Aidha, jengo la Budocan lililoko uwanja wa Amaan lililojengwa kwa ushirikiano unatumika kwa mchezo wa judo, karati pamoja na michezo mengine ya ndani.

Uwanja wa Gombani Pemba nao umefanyiwa marekebisho makubwa pamoja na kuezeka paa jipya ili kuwezesha kukidhi haja ya kutumika kwa mashindano ya Kimataifa. Uwanja huo pia uliongezewa haiba kwa kuwekwa taa kwa lengo

Dk. Shein pamoja na wanamichezo walioshiriki mashindano ya riadha Maisara

la kuufanya uweze kutumika pia kwa nyakati za usiku.

Katika kuuweka uwanja huo katika kiwango cha kimataifa, Wizara inayohusika na masuala ya Michezo hivi sasa imo katika harakati za kujenga njia ya kukimbilia kwa kutandika mpira (tartan) ili kutoa fursa ya michezo ya riadha kufanyika kwa ufanisi mkubwa. Lengo la harakati hizo ni kukamilika kwa kazi hiyo mwishoni mwa mwezi wa Desemba mwaka huu.

Aidha, kwa kushirikiana na Serikali ya Japan, kiwanja cha Gombani kimejengwa jengo jipya litakalotumika kwa ajili ya michezo ya ndani. Jengo hilo litatumika kwa mchezo wa judo, karati pamoja na michezo mengine ya ndani.

Sherehe za Bonanza la Michezo katika kiwanja cha Amani

Maoni ya Wananchi

Wanahabari kutoka sehemu tofauti walitembelea vijijini kupata maoni yao kuhusiana na utekelezaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya wamu ya saba hasa Rais wa Zanzibar kama inavyoonekana kwenye picha.

Uongozi wa Dk. Shein katika kipindi cha miaka minne umejenga mazingira mapya ya uwajibikaji kwa viongozi na watendaji pamoja na wananchi kufufua moyo wa kujitolea katika kuanzisha miradi yao ya maendeleo ili kupambana na hali ngumu ya umasikini.

Wanakijiji wa Ngomeni, Pemba;

Wananchi wa kijiji cha Ngomeni Shehia ya Mgelema Wilaya ya Chake Chake Kisiwani Pemba wameelezea kuridhishwa kwao na uongozi wa Dk. Shein kwa kuwa wenye mtazamo wa kusaidia maendeleo ya wananchi zaidi tofauti na baadhi ya viongozi wengine wa kisiasa ambao kwao suala la ubinafsi linaonekana wazi wazi.

Bw. Khamis Machano Ali mkaazi wa Ngomeni shehia ya Mgelema amesema “Kilio kikubwa cha wananchi wa Ngomeni kabla na baada ya mapinduzi kilikuwa ni ukosefu wa barabara, lakini kwa kipindi cha miaka minne tu ya uongozi wa Dk. Shein, sasa Ngomeni imekuwa na barabara ya uhakika ya kwenda na kurudi kijijini na kinachosuburiwa ni kuwekewa lami hatua ambayo naamini haitachukua muda iwapo hali ya uchumi itaendelea kuwa nzuri”.

Wananchi wa Chimba, Pemba;

Nao wananchi wa kijiji cha Chimba wilaya ya Wete wameuelezea mfumo wa Dk. Shein wa kufanya ziara za mara kwa mara kutembelea Wilaya na Mikoa na kukutana na kuzungumza ana kwa ana

na wananchi wanaojishughulisha na kazi za kilimo, ufugaji na sekta nyengine, kuwa ni mfumo ambao unahitaji kuigwa na viongozi wengine kwa lengo la kuharakisha maendeleo na ushiriki wa wananchi katika utekelezaji wa mipango na mikakati ya Serikali.

"Wananchi wa Chimba tulikuwa tumeshakata tamaa juu ya kufanikisha mradi wa ujenzi wa kituo chetu cha afya ulioanzishwa kwa nguvu za wananchi, lakini kitendo chake cha kuweka jiwe la msingi la kituo hicho na nasaha zake kwetu ni mambo yaliyofufua upya ari yetu na kutufanya kukamilisha ujenzi wa kituo chetu hicho kwa haraka", Alisema Maalim Hamad.

Wananchi wa Chanjaani, Pemba;

Kijana Salum Juma Salum mkaazi wa Chanjaani alitoa pongezi maalum kwa Dk. Shein kwa wazo lake la kufikiria kuanzisha Wizara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa lengo la kuongeza vipato kupitia makundi ya vijana na wanawake kwa kuzihusisha sekta za uvuvi, kilimo, ufugaji na kazi nyengine za mikono.

"Tuachane na ushabiki na mitizamo ya kisiasa, tukiweka ukweli na uwazi, Dk. Shein amekuwa ndiyo nuru ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar" alisema kijana Salum ambaye ni mjasiriamali.

Wananchi wa Kajengwa, Unguja;

"Zamani wananchi wa Kajengwa tulikuwa tukipata huduma za afya katika hospitali ya Koteji, Makunduchi, ambayo iko masafa marefu na kijiji chetu

Mahojiano ya waandishi wa habari na Sheha wa Shehia ya Ngomeni kisiwani Pemba

na tulikuwa tukipata usumbufu pale tunapohitaji kupata huduma hiyo, lakini ilikuwa ikitulazimu kufanya hivyo, sasa usumbufu huo umetuondoka baada ya kupata kituo cha afya kwenye kijiji chetu; tunamshukuru sana Dk. Shein", alisema Bwana Sigombe.

Wananchi wa Cheju, Unguja;

Bibi Hamida Mahamoud Mzee mkaazi wa kijiji cha Cheju ameielezea Cheju ya leo kuwa ni ya maendeleo na wananchi wamekuwa wakifaidika na huduma muhimu kama vile za barabara, maji na huduma za umeme ambazo alisema zinatokana na uongozi wa serikali ya awamu ya saba.

"Umaarufu wa kijiji chetu zamani ni kilimo cha mpunga mabondeni tofauti na leo ambapo wananchi wengi wameanza kushajiika kujenga nyumba kubwa za kuishi kufuatia kuimarika kwa huduma muhimu za kiuchumi na kijamii", alisema Bibi Hamida.

Wananchi wa Daya, Pemba;

Wananchi wa Shehia za Daya, Mtambwe Kusini na Kaskazini Wilaya ya Wete Mkoa wa Kaskazini Pemba wameishukuru na kuipongeza serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa kukamilisha ujenzi wa barabara zao na kuwafanya wananchi wa vijiji vya Shehia hizo kuwa na uhakika wa kusafirisha bidhaa na mazao yao.

Bwana Faki Abdalla Hassan Mkaazi wa Mtambwe Kaskazini alisema kukamilika kwa ujenzi wa barabara yao kutatoa fursa kwa wananchi wa ndani na nje ya

Mahojiano ya Rais na Waandishi wa habari katika kiwanja cha ndege cha Zanzibar

kijiji chao kuitumia vizuri barabara kwa kuongeza wingi wa vyombo vya kusafiria na kuwa kichocheo cha kuongeza maendeleo yao.

Bi Rehema Khamis Ahmada alisema kuwepo kwa barabara ya kisasa katika kijii cha Mtambwe Kaskazini ni ukombozi wa wanawake kwani akinamama wengi walikuwa wakiteseka na hali ya ubovu wa barabara uliokuwepo hasa wakati walipokuwa waja wazito au wakiwa na watoto wachanga.

Wananchi wa Ukunjwi, Pemba;

Wananchi wa Kijiji cha Ukunjwi Jimbo la Gando Wilaya ya Wete Kisiwani Pemba wameelezea kuridhishwa kwao na utekelezaji wa ahadi zinazotolewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa Kampeni za uchaguzi mkuu sambamba na ahadi anazozitoa wakati wa ziara zake za kutembelea wilaya na Mikoa mbali mbali ya Unguja na Pemba.

Wamesema juhudi kubwa zinazochukuliwa na Dk. Shein katika utekelezaji wa ahadi zake kwa wananchi zinastahili kupongezwa na kuungwa mkono na wananchi pamoja na viongozi wote wenye mtazamo wa kuwaletea maendeleo wananchi wao.

Naye Bibi Khadija Khamis Juma mkaazi wa shehia hiyo ya Ukunjwi amesema wananchi wa kijiji cha Ukunjwi sasa wanaweza kujiimarisha zaidi kufutia hatua ya kupatikana kwa umeme katika kijiji chao huduma ambayo imekuwa ukihitajika kwa miaka mingi.

Siri ya Mafanikio ya Dk. Shein

Je! Ni nini siri ya mafanikio ya Serikali ya awamu ya saba yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa iliyodumu madarakani kwa muda wa miaka minne sasa?

1. Uvumilivu wa kisiasa miongoni mwa viongozi wa ngazi za juu wanaounda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa.

2. Dhamira ya kweli ya kutekeleza kwa vitendo yale yote yaliyoahidiwa kwa wananchi kwa mujibu wa hali inavyoruhusu pamoja na Rais mwenyewe Dk. Ali Mohamed Shein kukutana na watendaji na wananchi mara kwa mara kuzungumzia mafanikio na changamoto ambazo Serikali inakabiliana nazo katika kutekeleza mipango yake ya maendeleo.

3. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuungwa mkono na wananchi waliowengi, wananchi kukubali kujituma, kuacha kutekeleza miradi yao kwa kutegemea misaada ya wafadhili, kukubali kufanyakazi kwa kujitolea kila inapotokezea haja ya kufanya hivyo.

4. Washirika wa maendeleo kuzitambua juhudi za Serikali na kuziunga mkono kwa kutoa misaada mbali mbali kila inapohitajika.

5. Kuweka vipaumbele kwa mambo muhimu zaidi na kuyaacha mengine yakisubiri baadae kulingana na uwezo wa rasilimali fedha na watu.

6. Kudhibiti matumizi ya fedha za umma.

Kimetayarishwa na Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu na kuchapishwa kwa mashirikiano na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa UNDP

P.O.BOX: 2422
Zanzibar – Tanzania
Phone: +255 223 081/5
Fax: 024 223 3722
Email: com_ikulu@ikuluzanzibar.go.tz